JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

# VITENDO VINAVYOKATAZWA NA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI SURA 278 TOLEO LA UREKEBU LA MWAKA 2023

Sheria ya Gharama za Uchaguzi Sura 278 inakataza vitendo vifuatavyo kabla na wakati wa mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa kwa mtu aliyetangaza au kufanya vitendo vinavyoonesha nia ya kushiriki katika mchakato wa uteuzi, wakati wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa, kampeni za uchaguzi na uchaguzi:

i. Kutoa fedha, mikopo au kitu chochote chenye thamani ili kumshawishi mtu kupiga au kutopiga kura.

ii. Kuahidi au kutoa ajira, wadhifa sehemu ya kazi ili kumshawishi mtu kupiga au kutopiga.

iii. Kutoa zawadi, mkopo, msaada, ahadi, kununua kitu chochote au kuingia makubaliano na mtu mwingine, ili kupata uteuzi.

iv. Kutoa au kuwezesha kupatikana kwa uteuzi kutokana na zawadi, mkopo, msaada, ahadi au makubaliano yaliyoingiwa baina ya wahusika.

v. Kulipa au kuwezesha kulipwa fedha ili zitumiwe kwa ajili ya hongo.

vi. Kupokea au kukubali kupokea fedha, zawadi, mkopo, msaada, ahadi, wadhifa au kitu chochote chenye thamani ili upige au usipige kura.

vii. Kupokea fedha au kitu cha thamani kutoka kwa mtu aliyepiga au ambaye hakupiga kura, baada ya kumshawishi kupiga au kutopiga kura.

viii. Kutoa, kulipia au kupokea chakula, vinywaji, burudani kwa njia ya rushwa ili kumshawishi mtu kupiga kura au kutopiga kura.

ix. Kulipa au kuingia mkataba wa kulipia kusafirisha wapiga kura.

x. Kutumia nyumba, ardhi, jengo au eneo lolote kinyume cha sheria.

orpptanzania

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi -
Mtaa wa Nzuguni A
S.L.P 2851 DODOMA

Tovuti yetu